TANGAZO LA SERIKALI NA. 366 la Tarehe 4/9/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*Zimetungwa chini ya vifungu 6 na 16 (1)*

---

## SHERIA NDOGO ZA (KODI YA MAJENGO) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA ZA MWAKA 2014

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za Mwaka, 2015 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-

"Manispaa" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Tabora,

" Mkurugenzi " maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora au mtu yeyote anayetekeleza makujumu ya Mkurugenzi.

" Kukadiria " maana yake kukadiria Kodi ya Majengo kulingana na Sheria Ndogo hizi,

" Eneo la Mjini Kati " ni eneo ambalo lipo ndani ya Manispaa na mipaka yake.

" Eneo la Pembezoni " ni eneo lililoko nje ya eneo la mjini kati.

" Jengo " maana yake ni nyumba au jengo lililopo ndani ya mipaka ya Manispaa

" Kiwango " maana yake ni kodi ambayo itatozwa kwenye jengo au nyumba chini ya Sheria Ndogo hizi,

" Daftari la Uthamini " maana yake ni orodha ya majengo au nyumba zilizofanyiwa uthamini chini ya Sheria Namba 2 ya Kodi ya Majengo 1983.

" Daftari la Uthamini la Nyongeza " maana yake ni orodha ya majengo au nyumba zilizofanyiwa uthamini baada ya kuandaa daftari la uthamini kwa minajili ya kufanya uthamini wa nyumba au majengo yote ambayo hayamo kwenye dafari la uthamini.

" Nyumba iliyojengwa kwa ubora na vifaa vya ujenzi vya Hali ya Juu " maana yake ni nyumba iliyojengwa kwa paa la zege au vigae vya kuezekea, dari ya jasi au mbao (T&G) au zege, kuta za matofali zilizomaliziwa kwa lipu na rangi pia

Usajili

4. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa jengo ndani ya eneo la Halmashauri kuhakikisha kwamba jengo lake limesajiliwa na Halmashauri, na kupewa namba maalumu ya utambuzi ya mlipa Kodi ya Majengo na namba hiyo ibandikwe sehemu ya wazi inayoonekana.

Wajibu wa mmiliki

5. Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki ambaye anamiliki jengo ndani ya Halmashauri;-

(a) kulipa kodi ya majengo kama ilivyoelekezwa kwenye

jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(b) kuhakikisha kuwa jengo lake limesajiliwa na kuingizwa kwenye orodha ya walipa kodi.

Wajibu wa kulipa kodi

6.-(1) Kila mmiliki wa jengo ambalo halijathaminiwa ndani ya eneo la Halmashauri atakuwa na wajibu wa kulipa kodi kama ilivyoanishwa katika jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Mmiliki wa mali inayostahili kulipiwa kodi ya jengo ndani ya Mamlaka ya Halmashauri ,na yenye thamani kama ilivyooneshwa katika orodha ya mali zilizofanyiwa uthamini au orodha ya nyongeza ya mali kama hizo,ilioandaliwa kwa mujibu wa Sheria za (Kodi ya majengo)za Mamlaka za Miji na kama ilivyotolewa katika Gazeti la Serikali atawajibika kulipa kodi ya asilimia sufuri nukta mbili tano(0.25%) ya thamani ya mali kama ilivyo katika orodha ya uthamini.

(3) Mmiliki wa mali inayostahili kulipiwa kodi ya jingo ndani ya Mamlaka ya Halmashauri,na ambayo haiko katika orodha ya mali zilizofanyiwa uthamini au orodha ya nyongeza ya mali kama hizo,kama ilivyo katika jedwali la Sheria Ndogo hizi,atawajibika kulipa kodi katika kiwango sawia(flat rate)au kama ilivyoainishwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kulipa kodi

7.Kiwango cha Kodi kinachotozwa chini ya kifungu cha 6(1) na (2) cha Sheria Ndogo hizi,kitalipwa Halmashauri ndani ya muda wa siku thelathini(30) au mwezi mmoja tangu kuanza kwa tarehe 01Julai ya kila Mwaka.

Wajibu wa wakala

8. Endapo kodi yoyote haitolipwa ndani ya muda stahiki,mmiliki atawajibika kulipa kiasi anachodaiwa pamoja na riba ya asilimia moja(1%)kwa kila Mwezi ambapo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa ya wakala

(3) Wakala yeyote ambaye:-

(a) atashindwa kuwasilisha Halmashauri kiasi cha Kodi alichokusanya;

(b) kwa makusudi atadai kutoka kwa mmiliki yeyote kiasi cha fedha kuzidi alichotakiwa kutozwa;

(c) kwa makusudi atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri;

(d) atashindwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kama Mkusanya Kodi chini ya Sheria Ndogo hizi.

atakuwa ametenda kosa na atashitakiwa mahakamani na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo pamoja kulipa hasara atakayokuwa ameisababishia Halmashauri.

Adhabu

9. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi mitatu jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

10. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

**JEDWALI LA KWANZA**

Viwango vya Kodi za Majengo kwa Majengo ambayo hayajathaminiwa

1. Makazi/Residental……………………………..…… Tshs 25,000/=
2. Makazi/Biashara/Residential Commercial……..… Tshs 30,000/=
3. Biashara/Commercial…………………………….. Tshs 80,000/=
4. Viwanda vikubwa/Heavy Indusrtry ……………... Tshs 4,000,00/=
5. Viwanda vidogo/Light Industry……..…………… Tshs1,500,000/=
6. Karakana/Workshop………………………………. Tshs600,000/=
7. Depot/Petrol and Fuel station……………………... Tshs1500,000/=
8. Guest houses/Bar…………………………………. Tshs 150,000/=
9. Ghala,Godown/Ware house………………………. Tshs 800,000/=

10. Hotel………………………………………………. Tshs 300,000/=
11. Makazi ghorofa moja(Double storey)……………. Tshs 250,000/=
12. Makazi zaidi ya ghorofa moja…………………….. Tshs 500,000/=
13. Biashara ghorofa moja(Double storey)…………… Tshs 500,000/=
14. Biashara zaidi ya ghorofa moja…………………… Tshs 750,000/=

**JEDWALI LA PILI**

**FOMU YA KUFIFILISHA KOSA**

(Chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi…………………………………………………………… …………… wa SLP………………………… ninaefanya biashara ya ………………………………………………… katika eneo la ………………………………… lililopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora Nakiri kuwa leo tarehe ……………………………………Nilikiuka kifungu cha …………………………………………cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Majengo) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za mwaka 2014. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini …………………………………………………………

Mbele yangu…………………………………………………… (jina)

Saini ……………………………………………………………

Wadhifa ………………………………………………………